بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ



# CHUKUA TAHADHARI DHIDI YA NJAMA ZA SHETANI !

ومن مكايده أنه يأمرك أن تلقى المساكين وذوي الحاجات بوجه عبوس، ولا تُريهم بشرًا ولا طلاقة، فيطمعوا فيك، ويتجرأوا عليك، وتسقط هيبتك من قلوبهم، فيحرمك صالح أدعيتهم، وميل قلوبهم إليك، ومحبتهم لك؛ فيأمرك بسوء الخلق، ومنع البِشر والطلاقة مع هؤلاء، وبحسن الخلق والبِشْر مع أولئك، ليفتح لك باب الشر، ويغلق عنك باب الخير.

Amesema imamu Ibnul Qayyim, Allah amrehemu: (( Na miongoni mwa njama za shetani juu yako ni kukuamrisha ukutane na masikini na wenye haja mbalimbali kwa uso uliokunjana na wala usiwaonyeshe furaha wala uchangamfu ili wasije kutumaini (kupata chochote kutoka) kwako, na ili wasije kupata ujasiri (wa kukuomba) na ili isije kuvunjika (hali ya) kuogopeka kwako katika nyoyo zao. Jambo hilo linakunyima dua zao njema, na mioyo yao kukuelekea , na mapenzi yao kwako. Basi shetani kwa hilo (alilolifanya kwako) anakuwa amekuamrisha tabia mbaya na amezuia furaha na uchangamfu (unaotakiwa) pindi unapokuwa pamoja na masikini na wenye haja, na pia amekuzuia na tabia njema (unapokuwa) pamoja nao ili akufungulie mlango wa shari na aufunge mlango wa kheri kwako.

ومن كيد عدو الله تعالى : أنه يخوف المؤمنين من جنده وأوليائه فلا يجاهدونهم ولا يأمرونهم بالمعروف ولا ينهونهم عن المنكر وهذا من أعظم كيده بأهل الإيمان وقد أخبرنا الله تعالى سبحانه عنه بهذا قال : إنما ذلكم الشيطان يخوف أولياءه فلا تخافوهم وخافون إن كنتم مؤمنين [ آل عمران : 175 ] المعنى عند جميع المفسرين : يخوفكم بأوليائه قال قتادة : يعظمهم في صدوركم ولهذا قال فلا تخافوهم وخافوني إن كنتم مؤمنين فكلما قوي إيمان العبد زال من قلبه خوف أولياء الشيطان وكلما ضعف إيمانه قوي خوفه منهم ومن مكايده أنه يسحر العقل دائما حتى يكيده ولا يسلم من سحره إلا من شاء الله فيزين له الفعل الذي يضره حتى يخيل إليه أنه من أنفع الأشياء وينفر من الفعل الذي هو أ نفع الأشياء له حتى يخيل له أنه يضره فلا إله إلا الله كم فتن بهذا السحر من إنسان وكم حال به بين القلب وبين الإسلام والإيمان والإحسان وكم جلا الباطل وأبرزه في صورة مستحسنة وشنع الحق وأخرجه في صورة مستهجنة ....))

'Na miongoni mwa njama za adui wa Allah (ambaye ni shetani) ni kuwahofisha waumini dhidi ya jeshi lake na vipenzi wake (katika majini na watu), mpaka waumini wakawa si wenye kupambana nao na wakawa hawawaamrishi wema wala kuwakataza uovu (kwa sababu ya kuwaogopa) , na hii ni miongoni mwa njama kubwa mno (anayoifanya shetani) kwa waumini . Na hakika Allah ameeleza kuhusu hili akasema: (( Hakika huyo ni shetani kwenu ambaye anawahofisheni dhidi ya vipenzi wake , basi msiwaogope bali niogopeni mimi ikiwa ninyi ni waumini wa kweli)) Aal Imraan 175. Maana ya aya hii kwa wanachuoni wote wa tafsiri ni kama alivyosema Qataadah ; 'Shetani anawatukuza vipenzi wake katika mioyo yenu, na ndio maana Allah akasema msiwaogope (msiwatukuze) bali niogopeni mimi ikiwa ninyi ni waumini wa kweli.' Kadiri imani ya mtu inavyokuwa madhubuti ndivyo inavyoondoka hofu ya vipenzi wa shetani, na kadiri inavyodhoofu imani ya mtu ndivyo inavyoimarika hofu yake dhidi ya vipenzi wa shetani.

Na miongoni mwa njama za shetani , ni kuipumbaza na kuilewesha (kuiroga) akili mpaka akainasa, na hakuna aliyesalimika dhidi ya uchawi wake isipokuwa yule ambaye Allah amemtaka. Shetani huipambia nafsi jambo lenye madhara kwa mtu mpaka akamdhanisha kuwa jambo hilo ndilo lenye manufaa zaidi, na shetani huichukiza nafsi katika jambo lenye manufaa kwa mtu mpaka akamdhanisha kuwa jambo hilo lina madhara makubwa kwake; LAAILAAHA ILLA LLAAHU, ni watu wengi kiasi gani ambao wamefitinika kwa uchawi huu wa shetani ! Na watu wengi kiasi gani ambao uchawi huu umezuia baina ya mioyo yao na uislamu na imani na wema ! Na watu wengi kiasi gani wameifunua batili na wakaianika wazi kwa sura yenye kupendeza na wakaiponda haki na wakaidhihirisha kwa sura mbaya ! ))

MWISHO

المصدر: إغاثة اللهفان في مصايد الشيطان

وصلى الله على محمد وعلى آله وصحبه وسلم

Mkusanyaji na Mkalimani: Ummati Abdallah, Abuu Muhammad